TVET CERTIFICATE III

# KISWAHILI WASTANI

CCMKK301

Kutumia **Kiswahili Wastani**

Competence

**Idadi ya vipindi:3**

**Saa zinazofaa: 30**

**Idara: Zote**

**Mikondo:Yote**

**Wakati ilipoandaliwa:** Oktoba, 2020

**Lengo**

**Moduli hii inaeleza ujuzi na uwezo vinavyostahiliwa ili mwanafunzi aweze:**

- Kutumia Kiswahili wastani kwa kusikiliza, kusoma, kuzungumza na kuandika katika shughuli za kazi;
- Kutumia herufi kimaandishi na kimazungumzo kwa kuzingatia lafudhi na shada za Kiswahili;
- Kuwasilisha habari/ujumbe kimazungumzo na kimaandishi kwa kuzingatia matumizi ya nyakati za Kiswahili;
- Kuwasilisha habari/ujumbe kimazungumzo na kimaandishi kwa kuzingatia matumizi ya aina za maneno ya Kiswahili

YALIYOMO


| Kitengo na vigezo vya kitengo | | Uk. |
|---|---|---|
| Kitengo | Vigezo vya kitengo | |
| 1._Kitengo cha 1 – Kutumia herufi za Kiswahili katika maandishi na mazungumzo | 1.1. Matamshi ya herufi za Kiswahili. | 3 |
| | 1.2 .Uwezo wa kusoma maneno yanayoandikwa. | |
| | 1.3.Uwezo wa kuandika maneno na sentensi anavyoambiwa. | |
| 2.Kitengo cha 2 – Kutumia kimaandishi na kimazungumzo nyakati za Kiswahili | 2.1. Uwezo wa kutumia nyakati zinazofaa katika sentensi ya kimazungumzo. | 7 |
| | 2.2. Matumizi ya nyakati zinazofaa katika sentensi za kimaandishi. | |
| | 2.3.Matumizi ya vimbishinyakati na viambishinafsi katika sentensi sahihi( kimazungumzo na kimaandishi). | |
| 3. Kitengo cha 3 – Kutumia kimazungumzo na kimaandishi aina za maneno ya lugha ya Kiswahili | 3.1. Uwezo wa kutunga tungo sahihi kwa kutumia aina mbalimbali za maneno kimazungumzo na kimaandishi. | 12 |
| | 3.2. Uwezo wa kuelewa tungo zilizotolewa na mtu mwingine zikitumia iana mbalimbali za maneno ya Kiswahili. | |
| | 3.3.Uwezo wa kutunga sentensi kulingana na upatanisho wa kisarufi kimazungumzo na kimaandishi. | |

# Kitengo cha 1 – Kutumia herufi za Kiswahili katika maandishi na mazungumzo

## Yanayotegemewa 1.1 – Matamshi ya herufi za Kiswahili kwa kuzingatia lafudhi

- Irabu , Konsonanti na mwambatano wa konsonanti

Lugha ya Kiswahili ina herufi za alfabeti ishirini na nne (24). Herufi hizo zinagawanyika katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni irabu (vokali) tano (5). Kundi la pili ni konsonanti kumi na tisa (19).

Alfabeti hizo zote ni hizi zifuatazo: **a,b,c,d,e,f,g,h,i,j,k,l,m,n,o,p,r,s,t,u,v,w,y,z.**

**Irabu au vokali**

Irabu za Kiswahili ni tano. Matamshi yake ni kama yale ya lugha ya Kinyarwanda.

Mfano: **a : a**cha, **a**ngalia

**e : e**ndelea, **e**mbe

**i : i**ngia, **i**mba

**o : o**ndoka, **o**ndoa, **o**na, **o**rodha

**u :u**kuta, **u**limi, **u**fagio, **u**dongo, **u**fa, **u**ma, **u**kuta

**Konsonanti**

Konsonanti zinazotumiwa katika lugha ya Kiswahili ni kumi na tisa.

**Mifano:**

**b** : baba, babu, bibi, bubu

**c :** herufi hii, haitumiwi peke yake, kila mara hufuatana na «**h**»**.** hivyo hugeuka «**ch**».

Chuchu, chache, chotara, chura, chumba

**d** : dada, daftari, daktari, dari, debe

**f** : faida, fahali, faini,faranga, farasi, kifafa

**g** : goti, godoro, gorofa, gori, gazeti, gereza, goigoi

**h** : habari, hawara, hawala(cheki,hundi), hekima(akili,busara,ujuzi), herufi,hekalu,homa,hotuba

**j :** juma, joto, jina, jambazi, jana, jangwa, jela, jua

**k** : kaka, karamu, kalamu, kazi, katikati, karatasi, kiroboto

**l :** lazima, labda, lengo, leo, laini, laana, lakini, lisani, lofa, luteni, lusu(mwizi)

**m** : mama, mwizi, maziwa, mate, miwani, misa, moshi, moto, motokaa, mume

**n** : nini,nani, noma(kipingamizi), noeli, novemba, nuru

**p** : pua, papa, pasaka, paredi, pasi, pasipoti, papai,pole

**r** : ruhusa,rais, roho, rafiki, rajabu, raia,rehema, refa,riziki

**s :** sisi, samba,sita, sifa,sauti, sasa, soko, safari, sakafu, sufuria, sarufi, sekondari, serikali,sufuri

**t** : tano,tatu, timu, tembo(ndovu), tabia, takataka, tarafa, tupu, tundu

**v** : viti, vita, vibaya, vitamini, vokali, visu,vizuri

**w** : watu, waridi, wao, wakati,wapi, wewe, wilaya, wazazi, wawili,wezi, wimbo, waraka

**y** : yeye, Yohana, yale, yai, yaya, Yesu, yatima, Yule

**z** : zeze, zizi, zamani, zahanati, zaidi, ziada, zimwi, zawadi

Isipokuwa irabu na konsonanti, lugha ya Kiswahili huwa na vitamkwa vinavyotokana na mfuatano au muungano wa konsonanti zaidi ya moja. Vitamkwa hivyo ni vifuatavyo:

**dh, th, ch, ng', gh, ng, nn, mbw, mch, ny, sh, n.k**

**Mifano:**

**dh:** fedha, dhambi, dhahabu, dhoruba, dharau, udhaifu, n.k

**th:** thelathini, themanini, thamani, themometa, theluthi, n.k

**ch:** chakula, mchezo, chimbuko, chotara, machozi, chura, chache, n.k

**ng': kitamkwa hiki huwa na sauti ya pekee inayokaribia kufanana na jinsi tunavyotamka «nk» katika lugha ya Kinyarwanda.**

ng'ombe, ng'onzi(kondoo), ng'ambo, ng'ang'ania, n.k

**ng:** ngozi, ngoma, ngano, nguruwe, ngamia, nguvu, n.k

**gh:** lugha, gharama, ghasia(fujo), ghala(stoo,bohari), ghadhabu(hasira, hamaki, ghaidhi, mafutu), ghafla, n.k

**nn:** nne

**mbw:** mbwa, mbweha(bweha)

**mch:** mchana, mchaguzi, mchaichai, mchakamchaka, mchoraji, mchumba, n.k

**ny:** nyanya, nyama, nyani, nyati(mbogo), nyumba, nyuma, nyonyo(chuchu), n.k

**sh:** shati, shule, shughuli, shuka, shingo, sherehe

## Yanayotegemewa 1.2 – Uwezo wa kusoma maneno yanayoandikwa

- Maana ya istilahi

1. Silabi: Ni kipashio cha kifonolojia kinachohusu matamshi ambapo sauti za lugha hutamkwa mara moja kwa pamoja kama fungu moja la sauti.Kila neno hufanywa na silabi. Kama silabi inaishia kwa konsonanti inaweza kuitwa **silabi iliyofungwa(silabi funge)**,kama inaishia kwa vokali inaweza kuitwa **silabi wazi(silabi huru).**

   **Mifano:**

   **a) Mifano ya maneno yenye silabi moja**

   - Tu
   - Na

   **b) Mifano ya maneno yenye silabi mbili au zaidi**

   - Ne-n-da
   - Ku-ja
   - Shu-le
   - Ma-a-na
   - Ra-fi-ki
   - Se-ri-ka-li, n.k.....

2. Mofimu: Ni kipashio kidogo kuliko vyote katika lugha chenye maana ya kisarufi/kileksika.Mofimu katika sarufi ni jina la sehemu ndogo kabisa yenye kuwakilisha ujumbe maana katika neno.kipashio hiki hakiwezi kuvunjwavunjwa zaidi bila kupoteza maana

   Kwa mfano neno **analima**- a-na-li-ma. Neno analima lina **mofumu nne** ambazo hufungamana na kujenga neno analima.

   Aina za mofimu

   - **Mofimu huru**

Ni silabi moja au zaidi yenye maana kamili ya neno na inaweza kujisimamia bila msaada wa viambishi au silabi nyingine.

Kwa mfano:

i) Daktari

ii) Nyumba

iii) Ndoa

- **Mofimu tegemezi/funge/ambata**

Mofimu tegemezi huhitaji viambishi au mofimu tegemezi ili kuleta maana iliyokusudiwa.

Kwa mfano: **wa-me –tu-sumbu-a**

- **Wa-** kiambishi kiwakilishi cha nafsi ya tatu katika wingi
- **-me-** kiambishi cha wakati timilifu
- **-tu-** kiwakilishi cha nafsi ya kwanza aktika wingi-kitendewa/nafsi mtendwa
- -**sumbu-** shina la kitenzi kusumbua
- **-a**: Kimalizio/kiishio

3. Fonimu: Ni tamshi katika neno ambalo likibadilishwa na tamshi jingine maana ya neno hilo hubadilika au hupotoka katika lugha hiyo. K.m: **sabuni** na **zabuni** hapa fonimu zinazotofautisha maana ni /**s**/ na /**z**/
4. Kiambishi: Ni kipande cha neno, aghalabu huwa ni silabi,kinachoweza kuambatishwa kwenye mzizi wa neno na kuunda neno jipya:'-**ni'** ni kiambishi cha mahali katika maneno 'shamba**ni**' na 'darasa**ni**'
5. Shadda/Mkazo(**stress**): Ni maneno yanayotumika kutilia mkazo au kusisitiza hali fulani. Ni mkazo unaowekwa kwenye silabi fulani ya neno ikiwa imetamkwa kwa msisitizo.
6. Kiimbo( **intonation**):Ni jinsi sauti inavyopanda na kushuka mtu anapoongea
7. Lafudhi : Ni upekee wa mtu katika matamshi (accent) unaoathiriwa na lugha ya mama, mazingira yake ya kijiografia au kiwango ujuzi wake wa lugha.

**Yanayotegemewa 1.3 – Uwezo wa kuandika maneno na sentensi vinavyosomewa.**

- Mifano ya sentensi

1. Vijana wanacheza mpira
2. Mwalimu anafundisha wanafunzi
3. Viwanda vitano vya nguo ambavyo viko chini ya Shirika la Nguo la Taifa vinakabiliwa na upungufu mkubwa wa dawa.
4. Jastini anaandika barua
5. Amina anakwenda dukani
6. Mgeni wetu atalipanda gari lile
7. Mwanafunzi mwema alikisoma kitabu hiki
8. Mkulima hodari aliipanda miti ile mirefu
9. Dereva mwangalifu aliliendesha basi hili
10. Lena alizianua nguo alizozianika ukambaani.

## Kitengo cha 2 – Kutumia kimaandishi na kimazungumzo nyakati za Kiswahili

**Yanayotegemewa 2.1 – Uwezo wa kutumia nyakati zinazofaa katika sentensi za kimazungumzo.**

- Matumizi ya nyakati katika Kiswahili

Wakati, katika Kiswahili huonekana katika vitenzi. Huonyeshwa na viambishi au viwakilishi wakati ndani ya kitenzi. Katika Kiswahili kuna nyakati tano:

i. Wakati uliopo -**na**-
ii. Wakati ujao -**ta**-
iii. Wakati uliopita-**li-**
iv. Wakati wa mazoea-**hu**-
v. Wakati uliotimilika -**me**-

I. **WAKATI ULIOPO (-na-)**

**Mfano:** Kitenzi kupika

| Tungo yakinishi | Tungo kanushi |
|---|---|
| Mimi ninapika chakula | Mimi sipiki chakula |
| Wewe unapika chakula | Wewe hupiki chakula |
| yeye anapika chakula | Yeye hapiki chakula |
| Sisi tunapika chakula | Sisi hatupiki chakula |
| Nyinyi mnapika chakula | Nyinyi hampiki chakula |
| Wao wanapika chakula | Wao hawapiki chakula |

TANBIHI:

1. Wakati uliopo unatumika kwa kueleza tendo linalotendeka sasa hivi, saa hizi, muda huu. Ni wakati wa sasa.
2. Kuweka kitenzi katika hali yakinishi ni kuchukua Kiambishi nafsi huru+ kiambishi nafsi ambatano+ na+ kitenzi kilichopoteza(ku).

II. **WAKATI UJAO** (-**TA**-)

**Mfano:** Kitenzi kupika

| Tungo yakinishi | Tungo kanushi |
|---|---|
| Mimi ni**ta**pika chakula | Mimi sitapika chakula |
| Wewe u**ta**pika chakula | Wewe hutapika chakula |
| Yeye a**ta**pika chakula | Yeye hatapika chakula |
| Sisi tu**ta**pika chakula | Sisi hatutapika chakula |
| Nyinyi m**ta**pika chakula | Nyinyi hamtapika chakula |
| Wao wa**ta**pika chakula | Wao hawatapika chakula |

**TANBIHI:**

1. Wakati huu, hutumika kwa kueleza vitendo vitakavyofanyika wakati utakaokuja baadaye (future tense)

2. Kuweka kitenzi katika hali yakinishi ni kuchukua Kiambishi nafsi huru+ kiambishi nafsi ambatano+ ta+ kitenzi kilichopoteza(ku).
3. Maneno yanayoonyesha wakati ujao ni: **kesho,keshokutwa, mtondo,mtondogoo**,n.k

III. **WAKATI ULIOPITA (-LI-)**

Viambishi wakati katika wakati uliopita ni –**li**- katika hali yakinishi na -**ku**- katika hali ya kukanusha.

Mfano:

Kitenzi:kupika

| **Tungo ya kinishi** | **Tungo kanushi** |
|---|---|
| Mimi nilipika chakula | Mimi sikupika chakula |
| Wewe ulipika chakula | Wewe hukupika chakula |
| Yeye alipika chakula | Yeye hakupika chakula |
| Sisi tulipika chakula | Sisi hatukupika chakula |
| Nyinyi mlipika chakula | Nyinyi hamkupika chakula |
| Wao walipika chakula | Wao hawakupika chakula |

**TANBIHI:**

1. Wakati huu, hutumika kwa kueleza vitendo vilivyofanyika zamani (past tense)
2. Kuweka kitenzi katika hali yakinishi ni kuchukua kiambishi nafsi huru+ kiambishi nafsi ambatano+ li+ kitenzi kilichopoteza (ku)
3. Maneno yanayoonyesha wakati uliyopita ni **: jana,juzi,juzijuzi,majuzi yale**

**IV. WAKATI ULIOTIMILIKA (-ME-)**

Katika wakati uliotimilika tungo yakinishi, kiambishi wakati ni **-me-.** Katika wakati uliotimilika, tungo kanushi, kiambishi wakati ni **-ja**-. Maneno yanayoonyesha wakati timilifu ni **leo** na **hivi punde**

**Mfano:** Kitenzi: kufungua

| **Tungo yakinishi** | **Tungo kanushi** |
|---|---|
| Mimi ni**me**fungua chupa | Mimi si**ja**fungua chupa |
| Wewe u**me**fungua chupa | Wewe hu**ja**fungua chupa |
| Yeye a**me**fungua chupa | Yeye ha**ja**fungua chupa |
| Sisi tu**me**fungua chupa | Sisi hatu**ja**fungua chupa |
| Nyinyi m**m**efungua chupa | Nyinyi ham**ja**mefungua chupa |
| Wao wa**me**fungua chupa | Wao hawa**ja**fungua chupa |

**TANBIHI**:

**1**.Kuweka kitenzi katika hali yakinishi ni kuchukua Kiambishi nafsi huru+ kiambishi nafsi ambatano+ **me**+ kitenzi kilichopoteza(ku).

V. **WAKATI WA MAZOEA (HU-)**

Katika wakati wa mazoea, kiambishi **-hu-** huchukua nafasi ya kiambishi nafsi na kiambishi wakati. Wakati wa mazoea humaanisha kutendeka kwa tendo kila siku au kila wakati.Katika kukanusha ni kama vile katika wakati uliopo.

**Mfano:** Kitenzi kutandika

| **Hali yakinishi** | **Hali kanushi** |
|---|---|
| Kila siku mimi hutandika kitanda | Kila siku mimi sitandiki kitanda |
| Kila siku wewe hutandika kitanda | Kila siku wewe hutandiki kitanda |
| Kila siku yeye hutandika kitanda | Kila siku yeye hatandiki kitanda |
| Kila siku sisi hutandika kitanda | Kila siku sisi hatutandiki kitanda |
| Kila siku nyinyi hutandika kitanda | Kila siku nyinyi hamtandiki kitanda |
| Kila siku wao hutandika kitanda | Kila siku wao hawatandiki kitanda |

**TANBIHI**:

Kuweka kitenzi katika hali yakinishi ni kuchukua kiambishi nafsi huru+ **hu**+ kitenzi kilichopoteza(ku). Hali kanushi ni kama wakati uliopo.

## Yanayotegemewa 2.2 – Matumizi ya nyakati zinazofaa katika sentensi za kimaandishi.

- Matumizi ya nyakati katika sentensi

**MIMI NA YOZEFU**

Jana, mimi na Yozefu tu**li**kwenda sokoni. Sokoni tu**li**nunua vitunguu, chumvi, pilipili, viazi vitamu, maharage na ndizi. Sisi **hu**la viazi na maharage.

Leo asubuhi tu**me**kwenda sokoni tena. Lakini **hatuku**nunua vitu vingi. Leo tu**me**nunua sabuni ya kufulia na sabuni ya kuogea. Sasa mimi ni**na**kwenda dukani kununua sigara na kiberiti. Baba **hu**vuta sigara lakini Mama havuti. Baba **hu**nituma dukani kila siku. Juzi a**li**nituma kununua wembe lakini jana **haku**nituma wembe. Jana Mama a**li**nituma mimi na Yozefu kwenda sokoni.

Kesho mimi na dada tu**ta**kwenda shuleni. **Hatuta**kwenda sokoni wala dukani. Tu**ta**kwenda shuleni kusoma. Tukitoka shuleni tu**ta**rudi upesi nyumbani. Baba yangu ni seremala, na Mama **hu**fanya kazi ya nyumbani. Hivi ni**ta**msaidia Mama kazi za jikoni. Dada **hata**msaidia Baba.

## Yanayotegemewa 2.3 – Matumizi ya viambishinyakati na viambishinafsi katika sentensi sahihi

- Viambishi nyakati

| KIAMBISHI | WAKATI/MATUMIZI |
|---|---|
| 1.- na- | Wakati uliopo |
| 2. -li- | Wakati uliopita |
| 3. -ta- | Wakati ujao |
| 4.-me- | Wakati timilifu |
| 5.hu- | Wakati wa mazoea |

- Viambishinafsi

VIAMBISHI NAFSI HURU

| Nafsi | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| Nafsi ya 1 | Mimi | Sisi |
| Nafsi ya 2 | Wewe | Nyinyi/ ninyi/ nyie |
| Nafsi ya 3 | Yeye | wao |

- VIAMBISHI NAFSI AMBATANO

| **Nafsi** | **Umoja** | | **Wingi** | |
|---|---|---|---|---|
| | Yakinishi | Kanushi | Yakinishi | Kanushi |
| Nafsi ya 1 | Mimi ni ... | Mimi si... | Sisi tu... | Sisi hatu... |
| Nafsi ya 2 | Wewe u.... | Wewe hu... | Nyinyi m... | Nyinyi ham... |
| Nafsi ya 3 | Yeye a.... | Yeye ha... | Wao wa... | Wao hawa... |

**Tanbihi**: Katika Kiswahili nafsi zinaweza kutajwa kwa mkato.

**Mifano:**

1. Wewe na mimi: Wewe nami
2. Nyinyi na sisi: Nyinyi nasi
3. Yeye na wewe: Yeye nawe
4. Wao na nyinyi: Wao nanyi
5. Mimi na wao: Mimi nao
6. Sisi na wao: Sisi nao

## Kitengo cha 3 – Kutumia kimazungumzo na kimaandishi aina za maneno ya lugha ya Kiswahili

**Yanayotegemewa 3.1 – Uwezo wa kutunga tungo sahihi kwa kutumia aina mbalimbali za maneno kimazungumzo na kimaandishi.**

- Aina za maneno ya Kiswahili

Aina za maneno ya Kiswahili ni:

i) Nomino
ii) Vivumishi
iii) Viwakilishi
iv) Vielezi
v) Viunganishi
vi) Vihisishi
vii) Vihusishi
viii) Vitenzi

### i) NOMINO

Nomino ni maneno ambayo hutaja vitu. Kwa hiyo nomino hutaja majiana ya watu,vitu,vyeo, dhana na hata tendo.

Aina za nomino

**a) Nomino za pekee**

Ni nomino ambazo hutaja vitu vya pekee. Kitu cha pekee ni kitu mahususi na ni cha pekee kwa sababu kipo chenyewe tu hapa duniani.Nomino za pekee hutaja majina ya:

1. **Watu**: Juma, Omari , Tumaini, Kamana, Peter, n.k..
2. **Miji**: Nairobi, Kigali, Dodoma,n.k.....
3. **Nchi** : Rwanda, Uganda, Tanzania,n.k..
4. **Mito**: Akagera, Tana, Nile, Aakanyaru,n.k...
5. **Milima** : Kilimanjaro, Everest, Muhabura,n.k...
6. **Maziwa**: Kivu, Tanganyika, Victoria, Ruhondo, Muhazi,n.k...
7. **Bahari**: Hindi, Atlantiki,n.k..
8. **Miezi**: Machi, Juni, Oktoba,n.k.....
9. **Siku za wiki**: Jumatatu, Ijumaa, Jumamosi, n.k....

**b) Nomino za kawaida**

Ni nomino zinazotaja vitu vya kawaida ambavyo si vya pekee.Nomino hizi hutaja vitu ambavyo ni vingi hapa duniani. Nomino hizi zinaweza kuwa na umoja na wingi. **Kwa mifano :**

1. Kitabu/vitabu
2. Mtu/watu
3. Ukuta/kuta
4. Jicho/macho
5. Debe/madebe
6. Kitanda /vitanda, n.k....

**c) Nomino za dhahania**

Ni nomino ambazo huwakilisha vitu ambavyo havina umbo halisi.Hizi ni nomino ambazo hatuwezi kuzihisi kwa kutumia vyungo vyetu au hata kama tungetumia darubini.Nomino hizi hazishikiki,hazionekani,hazinusiki, hazionjeki ha hazisikiki

**Mifano:**

1. Wivu
2. Mawazo
3. Wema
4. Upendo
5. Chuki
6. Woga
7. Uvumilivu
8. Huruma
9. Ushindi
10. Furaha,n.k....

Haziwezi kupimwa kwa njia yoyote,lakini zinafikirika.

**d) Nomino za jamii**

Ni nomino ambazo ndani yake kuna vitu vingi; yaani imekusanya vitu vingi ndani yake.

**Mifano**: kikosi,jeshi, bunge,kamati,timu,n.k....

**e) Nomino zinazohesabika na zisizohesabika**

Nomino zinasohesabika ni zile ambazo kila mtu yeyote anaweza kuhesabu kama vile: **vitanda**, **nyumba, magari,ndege,kalamu,karatasi,viatu**,n.k.... ilhali zisizohesabika ni zile ambazo hatuwezi kuhesabu kama vile: **maji,maziwa, mafuta, hewa, moshi, umeme,harufu**,n.k.....

**ii) VIVUMISHI**

Kivumishi ni neno ambalo hueleza zidi juu ya nomino.Ni neno ambalo hufafanua kitu,hali,sifa au tendo linalowakilishwa na nomino.

**Mifano :**

1. Mtoto **mrefu**
2. Msichana **mrembo**
3. Kitu **kizuri**
4. watu **watano**

**Aina za vivumishi**

a) Vivumishi vya sifa
b) Vivumishi vionyeshi
c) Vivumishi viulizi

d) Vivumishi vya idadi

e) Vivumishi vimilikishi

f) Vivumishi visisitizi

**a) Vivumishi vya sifa**

Ni vivumishi ambavyo hueleza sifa fulani ya nomino inayovumishwa.

Mifano:

1. Mti mrefu
2. Chakula  kitamu
3. Mtoto mfupi
4. Viti virefu
5. Watoto wafupi,n.k....

**b) Vivumishi vionyeshi**

1. Ni vivumishi ambavyo hukuonyesha au  kukuashiria kilipo kitu,mtu au jambo.

Mifano:

1. Mtoto **yule**/watoto **wale**
2. Mwanafunzi **yule**/wanafunzi **wale**
3. Kitabu **hiki**/vitabu **hivi**
4. Kalamu **hii**/kalamu **hizi**
5. Mto **huu**/mito **hii**,n.k.....

**c) Vivumishi vya idadi**

Ni vivumishi ambavyo hututajia idadi ya nomino inayovumishwa.

Mifano :

1. Watoto **wawili**
2. Mti **mmoja**
3. Wanafunzi **wengi**
4. Walimu **wachache**
5. Nahodha **kumi**.n.k.....

d) **Vivumishi viulizi**

Ni vivumishi ambavyo hutumiwa pamoja na na nomino ili kuuliza juu ya nomino hiyo

Mifano:

1. Macho **mangapi?**
2. Mikono **ipi?**
3. Mtoto **yupi?**
4. Watoto **wangapi?,n.k...**

e) **Vivumishi vimilikishi**

Ni vivumishi ambavyo hueleza jinsi nomino inavyomilikiwa

Mifano:

1. Mtoto **wangu**/watoto **wetu**
2. Mwanafunzi **wako**/ wanafunzi **wenu**
3. Kiti **chake**/ viti **vyao**

f) **Vivumishi vya kusisitiza**

Ni vivumishi ambavyo hutumiwa ili kusisitiza juu ya nomino iliyotajwa.

Mifano:

1. Kitabu **chenyewe**
2. Mwanafunzi **mwenyewe**
3. Ng'ombe **mwenyewe**
4. Kalamu **yenyewe**

**iii) VIWAKILISHI**

Ni maneno ambayo hutumiwa badala ya nomino. Maneno hayo huwakilisha nomino.

**Aina za viwakilishi**

a) **Viwakilishi vya nafsi**

Ni viwakilishi ambavyo hukaa badala ya majina ya watu.

Mifano:

| NAFSI | |
|---|---|
| **UMOJA** | **WINGI** |
| 1. Mimi | Sisi |
| 2. Wewe | Ninyi/nyinyi |
| 3. Yeye | wao |

**b) Vivumishi vya sifa na viwakilishi vya sifa**

Mfano :

1. wanafunzi hodari walifaulu lakini **wavuvi** walishindwa

**c) Vivumishi vya idadi na viwakilishi vya idadi**

Mfano:

1. Watu watano walifariki na **kumi** wakajeruhiwa
2. Wagonjwa wengi wamepona lakini **wachache** bado wanatibiwa

**d) Vivumishi vionyeshi na viwakilishi vionyeshi**

Mfano:

1. Kiti hiki ni changu lakini **kile** pale ni chako

**e) Vivumishi visisitizi na viwakilishi visisitizi**

Mfano:

1. Mnunuzi mwenyewe wa kitabu hajafika na **chenyewe** sijui kipo wapi.

**f) Vivumishi viulizi na viwakilishi viulizi**

Mfano:

1. Watu wangapi wamepiga kura na **wangapi** hawajapiga?

**g) Vivumishi vimilikishi na viwakilishi vimilikishi**

Mfano:

1. Nyumba yenu ni ndogo lakini **yetu** ni kubwa tena inapendeza

**iv) VIELEZI**

Ni maneno ambayo hueleza zaidi juu ya kitenzi , kielezi kingine au kivumishi.

Mifano:

1. Mwizi alipigwa **sana**.
2. Amina ni mnene **sana**.
3. Mwalimu anaongea **upesi mno**.

**Aina za vielezi**

**a) Vielezi vya wakati**

Ni vielezi ambavyo hueleza wakati ambapo tendo fulani lilifanyika au halikufanyika.

Mifano:

1. Omondi atakuja **kesho**
2. Iddi atakuja **Jumatano**
3. Tutaondoka **kesho alasiri**
4. Alifika **jana usiku**
5. Ataondoka **Machi**
6. Baba yake alifariki **zamani**
7. Mama atatupa chakula **punde**

b) **Vielezi vya mahali**

Ni vielezi ambavyo hueleza mahali ambapo tendo fulani linafanyikia,lilifanyikia au litafanyikia.

Mifano:

1. Walimu wamekwenda **Nairobi**
2. Babake anaishi **Kigali**
3. Muhire anaishi **Burundi**
4. Amekwenda **kaskazini**

**c) Vielezi vya kiasi**

Ni vielezi ambavyo hueleza kiasi cha kutendwa kwa tendo fulani au kiasi cha uvumishi au uelezi.

Mifano:

1. Mtoto ameshiba **sana**
2. Dereva anaendesha **haraka mno**
3. Ayubu ni mrefu **kidogo**

**d) Vielezi vya namna**

Ni vielezi ambavyo hueleza namna/jinsi tendo linavyotendwa

Mifano:

1. Anatembea **upesiupesi**
2. Anatembea **harakaharaka**
3. Alikuja **polepole**
4. Amevaa **kizungu**
5. Anaimba **vibaya/vizuri**
6. Alipigana **kiume**

**e) Vielezi viigizi/onamatopia**

Ni vielezi ambavyo huigiza milio ya matendo yanayotendwa.

Kwa mfano:

1. Alianguka **pu!**
2. Mtoto amelala **fofofo**
3. Alitumbukia majini **chubwi!**
4. Amelowa **chepechepe**

**f) Vielezi viulizi**

Ni vielezi ambavyo huuliza juu ya tendo. Kwa mfano:

1. Mwalimu anafundisha **vipi**?
2. Mgonjwa amepelekwa **wapi**?
3. Kagabo atarudi **lini?**
4. **Nani** aliyemlea mgonjwa?
5. Roza analeta **nini?**

**V) VIUNGANISHI**

Ni maneno ambayo hutumiwa kuunganisha vipashio mbalimbali katika Lugha. Lugha ya Kiswahili ina viunganishi vingi, kwa mfano: **na,halafu,lakini,au,wala,ila,pia,tena,ili, kwa sababu, bila ya, isipokuwa, basi, kwa minajili, nk**..

Mifano:

1. Mama **na** mtoto wanapendana.
2. Chakula kinapikwa **lakini** bado hakijaiva.
3. Mwizi hana aibu **wala** huruma.
4. Tutoroke **lakini** turudi mapema.
5. Usirudie kuiba **pia** usitudanganye tena.
6. Nimekuandika barua **kwa minajili** ya kujua hali yako.
7. Nimekuja tuongee **ili** nipate ukweli wa mambo.
8. Amefanya alitakalo **bila ya** kustahi watu.
9. Magonjwa yote yana dawa **isipokuwa** UKIMWI .
10. Iwapo unaogopa kweli UKIMWI,**basi** jiepushe na uasherati.
11. Ndugu wale wanateta **pasipo** na sababu yoyote.

**VI) VIHISISHI**

Kihishi ni neno linalofahamisha jinsi mzungumzaji au mwamdishi anavyohisi au kujisikia moypni mwake. Neno hilo laweza kuwa mshituko,kiapo,kukubali,furaha,huzuni,mshangao au hisia nyingine yoyote. Kihisishi hufafanuliwa kwa matumizi ya alama hisi (**!**).Vihisishi ,aghalabu huwa mwanzoni mwa sentensi na ni nadra kuwa mwishini ingawa hufanyika hivyo.

Mifano:

a) **Vihishi vya furaha**: Ewaa!, Oyee!,Chabaa! Oyaa!,Shabash!
b) **Vihishi vya huzuni**: Pole!Hamadi! Makiwa!
c) **Vihisishi vya mshangao**:Lahaula! Kumbe! Salale!Ajabu! Ati!Eti!Masalala!Mama wee!, Mamangu ee!
d) **Vihisishi vya mshituko**: Afanalek! La !,Lo!,Alaa!Jamani! Aisee!
e) **Vihisishi vya kiapo**: Wallahi! Billahi! Haki ya Mungu!
f) **Vihishi vya kukubali**: Naam!Haya!Ehh! Ohoo!

Mifano katika sentensi:

1. **Ewaa!**Timu yetu imeibuka kuwa washindi.
2. **Pole!** ndiyo ulimwengu watu hupoteza wawapendao.
3. **Hamadi** ! Nataraji kikombe hakikuvunjika.
4. **Wallahi!**Tena naapa, mimi sikushirikiana na wao ng'o
5. **Lahaula!**Mbona siku hizi umechukua tabia isiyokuwa yako?
6. **Jamani!** Watu wamekuwa na roho ngumu hata kuchomana moto.
7. **Salale!**Unakula kana kwamba hujaona chakula maishani mwako.
8. **Kumbe!** Na wewe pia umo.
9. **Alaa!**watu wote hawapo nyumbani
10. **Ajabu**!kwamba mpaka sasa wataalamu hawajagundua dawa ya UKIMWI

VII) **VIHUSISHI**

Kihusishi ni neno ambalo kwa kawaida hutumiwa na nomino au kiwakilishi na ambalo huzihusisha kisarufi nomino na viwakilishi hivyo na maneno mengine. Miongoni mwa vihusishi vinavyotumika sana katika Lugha ya Kiswahili ni **kwa** na **na** ( ya kauli ya kutendwa)

Mifano :

1. Nilituma salamu **kwa** rafiki yangu.
2. Tulikwenda **kwa** mganga wa kienyeji.
3. Tutasafiri **kwa** ndeage hadi London.
4. Alikutwa amesimama karibu **na** nyumba
5. Pili hulipiwa ada ya shule **na** shangazi yake.
6. Watu wengi wameshikwa **na** Ukimwi.
7. Nchi zote duniani zimepatwa **na** janga la korona.
8. Tutanunua chakula **kwa** bei yoyote.
9. Sabina aliolewa **na** Muhamad kwa hiari yake.
10. Wachezaji wote walifuraha sana **kwa** ushindi walioupata
    Mifano mingine ni :
1. Tulisafiri **kwa** basi **kutoka** Nairobi **hadi/mpaka** Arusha
2. Tumekaa siku mbili **bila** chakula

3. Wazungu wengi maskini **kama** sisi
4. Ndoa **bila** upendo haidumu
5. Haishi **katika** nyumba yake

## Yanayotegemewa 3.2 – Uwezo wa kuelewa tungo zilizotolewa na mtu mwingine.

- Mifano katika kifungu cha habari

Kifungu :Maji

Maji ni muhimu sana kwa maisha na viumbe vyote. Wanadamu,wanyama na mimea huhitaji maji. Kwa ukweli maji ni uhai, na uhai umo katika katika maji. Mimea huhitaji maji ili ipate kukua vizuri. Lakini kila mti huhitaji maji kwa kiwango cha maalumu. Baadhi ya miti huhitaji maji mengi. Miti mingine huhitaji kiasi na kuna miti inayohitaji maji kidogo.

Wanadamu huhitaji maji kwa shughuli mbalimbali kama vile kunywa,kuogea,kufulia na kupikia. Halikadhalika, wao huhitaji maji kuzimia moto unapotokea.

Watu hupata kutoka kwa mvua na pia kwa njia nyingine mbalimbali. Vijijini na mashambani, maji aghalabu hupatikana kutoka visimani au mitoni. Maji hutekwa yakawekwa katika chombo na kubebwa juu ya kichwa au mgongoni. Maji majumbani huwekwa katika mtungi,debe, au pipa. Watu wengine hutumia mkokoteni aua magari kubebea maji iwapo wana madebe mengi.

Mijini ,baadhi ya watu huuza maji kwa maarasi. Pamoja na hayo,majumba mengi siku hizi yana maji.

- Sentensi zilizotolewa na mtu mwingine hupatikana katika nafsi ya tatu umoja na ya tatu wingi
- Sentensi pia zilizotolewa na mtu mwimgine hupatikana katika hali ya kuamuru
  Mifano: “ Tumieni madaftari yenu,” Umuhoza alituambia
- Sentensi zilizotolewa na mtu mwingine hueleweka wakati amabapo zimeshawekwa katika **usemi wa taarifa**.
  Mifano:
  a) “Tuonane sasa,” Alimwambia ( **usemi halisi**)
  Alitaka waonane wakati ule (**usemi wa taarifa**)
  b) “Ninaandika barua” Kalisa alisema ( **usemi halisi**)
  Kalisa alisema kuwa aliandika barua( **usemi wa taarifa**)

## Yanayotegemewa 3.3 – Uwezo wa kutoa sentensi kulingana na upatanisho wa kisarufi kimazungumzo na kimaandishi

- <u>Ngeli za majina</u>

**NGELI YA A- WA-**

**MATUMIZI YA NGELI YA A- WA(M-WA)**

| Umoja | | Wingi | |
|---|---|---|---|
| Mtu | analima | Watu | wanalima |
| Mzee | anakuja | Wazee | wanakuja |
| Ndege | anaruka | Ndege | wanaruka |
| Malaika | anasema | Malaika | wanasema |
| Kibogayo | analima | Vibogoyo | wanalima |
| Kiziwi | analima | Viziwi | wanalima |
| Mbuzi | anakula | Mbuzi | wanakula |
| Ng’ombe | anakula | Ngombe | wanakula |

Ngeli ya -a-wa hujumuisha majina yote kama vile watu, wanyama, ndege na Mungu, Mashetani, Malaika, Miungu n.k

**VIVUMISHI VYA NGELI YA A- WA-**

**1. Vivumishi vya kuonyesha**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Mwalimu huyu anaandika | Walimu hawa wanaandika |
| Mwalimu huyo anaandika | Walimu hao wanaandika |
| Mwalimu yule anaandika | Walimu wale wanaandika |

**2.Vivumishi vya kumiliki(sha)**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Punda wako amepotea | Punda wenu wamepotea |
| Mzee wako anakusalimu | Wzee wenu wanawasalimu |
| Shetani wako amekupotosha | Mashetani wenu wamewapotosha |
| Punda wangu amepotea | Punda wetu wamepotea |

| | |
|---|---|
| Mzee wangu anakusalimu | Wzee wetu wanatusalimu |
| Shetani wangu amekupatosha | Mashetani wetu wametupatosha |
| Punda wake amepotea | Punda wao wamepotea |
| Mzee wake anakusalimu | Wzee wao wanawasalimu |
| Shetani wake amempotosha | Mashetani wao wamewapatosha. |

**Tanbihi**: Katika vivumishi vya kumilikisha kuna majina ya ngeli ya -a-wa- ambayo hayafuati kanuni hiyo. Mengi mwa majina hayo ni yale yanayoonyesha uhusiano wa familia.

**Mfano:**

1. Hatusemi baba wangu au mama wangu tunasema baba yangu, baba yako baba yake, baba yetu, baba zetu, baba zenu, shangazi yangu,..

2.Kuna pia majina ya watu yasiyofuata kanuni ya ngeli hii kama jina jambazi (hilo, hili,..)

**3) Vivumishi vya kurejesha /kusisitiza**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Mimi mwenyewe nililima shamba | Sisi wenyewe tulilima shamba |
| Mtoto mwenyewe alikimbia | Watoto wenyewe walikimbia |
| Mwizi mwenyewe ni huyu | Wezi wenyewe ni hawa |

**4. Vivumishi vya kuuliza**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Mwanajeshi yupi amekufa? | Wanajeshi wapi wamekufa? |
| Msichana yupi ameolewa? | Wasichana wapi wameolewa? |
| Mwanafunzi yupi amechelewa? | Wanafunzi wapi wamechelewa ? |
| Kibogoyo yupi amepigwa? | Kibogoyo wapi wamepigwa? |
| Mbuzi yupi amekinjwa? | Mbuzi wapi wamekinjwa? |

**5)Vivumishi vya idadi**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Mwalimu mmoja | Walimu wawili |
| | walimu watatu |
| | Walimu wanne |

Walimu watano

Walimu -sita

Walimu -saba

Walimu wanane

Walimu - tisa

Walimu - kumi

**Tanbihi:** Nambari sita, saba, tisa na kumi hazibadiliki katika wingi; katika ngeli hii hazichukui kiambishi -wa-.

**6) Vivumishi vya sifa**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Ng'ombe mkubwa | Ng'ombe wakubwa |
| Mpishi mpole | Wapishi wapole |
| Daktari mzuri | Madaktari wazuri |
| Msichana mrembo | Wasichana warembo. |

**NGELI YA U-I-**

Baadhi ya majina ya ngeli hii ni majina ya miti, maumbile, viungo vya mwili, vifaa na matendo. Ngeli hii huchukua majina yote ambayo kwenye kitenzi huwa na kiambishi u- katika umoja, na i- katika wingi.

Yafuatayo ni baadhi ya majina ya ngeli hii: mti-miti, mkono-mikono, mchungwa-michungwa, mwili-miili, mswaki-miswaki, mlango-milango, msitu-misitu, mto-mito, msumari-misumari, mpera-mipera, mgongo-migongo, mgomba-migomba, mguu-miguu, mdomo-midomo, mlima-milima, mkondo-mikondo, mnazi-minazi, mkaba-mikaba, mkufi-mikufi,...

**Tanbihi:** - Katika ngeli hii kuna majina ya umoja tu kama: - Mpunga, muda (mpunga umelimwa, muda umekwisha) - Kuna vile vile majina yenye wingi tu, kama: miwani, mirathi,..

**MATUMIZI YA NGELI YA U-I-**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Mti umeanguka | Miti imeanguka |
| Mkono umevunjika | Mikono imevunjika |

| | |
|---|---|
| Mchungwa una faida | Michungwa ina faida |
| Mwili umechoka | Miili imechoka |
| Mlango umefungwa | Milango imefungwa |
| Mto umejaa maji | Mito imejaa maji |
| Msumari unapigiliwa | Misumari inapigiliwa |
| Mpera umejaa matunda | Mipera imejaa matunda |
| Mnazi umekatwa | Minazi imekatwa |

**VIVUMISHI VYA NGELI U-I-**

**a)Vivumishi vya kuonyesha**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Mlango huu umeharibika | Milango hii imeharibika |
| Mlango huo umeharibika | Milango hiyo imeharibika |
| Mlango ule umeharibika | Milango ile imeharibika |

**b) Vivumishi vya kumuliki**

| | |
|---|---|
| Mgomba wangu ulipandwa | Migomba yetu ilipandwa |
| Mgomba wako ulipandwa | Migomba yenu ilipandwa |
| Mgomba wake ulipandwa | Migomba yao ilipandwa |

**c) Vivumishivya kurejesha**

| | |
|---|---|
| Msitu wenyewe unaungua | Misitu yenyewe inaungua |
| Mlango wenyewe uliharibika | Milango yenyewe iliharibika |
| Mto wenyewe ni mkubwa | Mito yenyewe ni mikubwa |

**e) Vivumishi vya idadi**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Msumari mmoja | Misumari miwili |
| | Misumari mitano |
| | Misumari -sita |
| | Misumari -saba |

Misumari minane

Misumari -tisa

Misumari -kumi

Misumari mia moja

Misumari mingi

**f)Vivumishi vya kuuliza**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Mti upi umekatwa? | Miti ipi imekatwa? |
| Mchungwa upi umezaa matunda? | Michungwa ipi imezaa matunda? |
| Mguu upi umevunjika? | Miguu ipi imevunjika? |

**g) Vivumishi vya sifa**

| | |
|---|---|
| Mti mkavu | Miti mikavu |
| Mti mzuri | Miti mizuri |
| Mti mfupi | Miti mifupi |

**NGELI YA KI-VI**

Ngeli hii huchukua majina ya vitu pamoja na viungo vya mwili; imeitwa ngeli ya ki-vi- kwa sababu hutambulishwa na kiambishi **ki**- katika umoja na **vi**- katika wingi. Yafuatayo ni baadhi ya majina ya ngeli hii: Kisu-visu, kijiko-vijiko, kikapu-vikapu, kiuno-viuno, kichwa-vichwa, kisiginovisigino, kikombe-vikombe, kiti-viti, kiwiko-viwiko, kioo-vioo, chuma-vyuma, chumba-vyumba, chombo-vyombo, choo-vyoo,...

**MATUMIZI YA NGELI YA KI- VI**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Kikombe kimevunjika | Vikombe vimevunjika |
| Kisu kimepotea | Visu vimepotea |
| Kitabu kimechafuka | Vitabu vimechafuka |

| | |
|---|---|
| Kijiko kimeanguka | Vijiko vimeanguka |
| Choo kimejaa | Vioo vimejaa |
| Kiberiti kinawaka | Viberiti vinawaka |
| Chumba kilifunguliwa | Vyumba vilifunguliwa |
| Kiti kimekaliwa | Viti vimekaliwa |
| Kitambaa kitafuliwa | Vitambaa vitafuliwa |
| Chungu kinasafishwa | Vyungu vinasafishwa |

**VIVUMISHI VYA NGELI KI-VI**

a) **Vivumishi vya kuonyesha**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Kitabu hiki kinapendeza | Vitabu hivi vinapendeza |
| Kitabu hicho kinapendeza | Vitabu hivyo vinapendeza |
| Kitabu kile kinapendeza | Vitabu vile vinapendeza |

b) **Vivumishi vya kumiliki**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Kiti changu kimevunjika | Viti vyetu vimevunjika |
| Choo chako kimejaa | Vyoo vyenu kimejaa |
| Kiberiti chake kimekwisha | Viberiti vyao vimekwisha |

c) **Vivumishi vya kurejesha**

| | |
|---|---|
| Kioo chenyewe kimepasuka | Vioo vyenyewe vimepasuka |
| Chungu chenyewe kimetoboka | Vyungu vyenyewe vimetoboka |
| Kisu chenyewe kimenolewa | Visu vyenyewe vimenolewa |

d) **Vivumishi vya kuuliza**

| | |
|---|---|
| Kiberiti kipi kimewaka? | Viberiti vipi vimewaka? |
| Kiberiti gani kimewaka? | Viberiti gani vimewaka? |
| Kisu kipi ni kizuri? | Visu vipi ni vizuri? |

e) **Vivumishi vya idadi**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Kitabu kimoja kimeibwa | Vitabu viwili vimeibwa |

Vitabu vitatu vimeibwa

Vitabu vine vimeibwa

Vitabu vitano vimeibwa

Vitabu sita vimeibwa

**f) Vivumishi vya sifa**

| | |
|---|---|
| Kitabu kizuri | Vitabu vizuri |
| Kitambaa kirefu | Vitambaa virefu |
| Kisu kipya | Visu vipya |

**NGELI YA LI-YA-**

Majina yanayoingia katika ngeli hii huwa na umoja na wingi. Wingi wa majina ya ngeli hii hupatikana kwa kupachikwa viambishi ma-. Yafuatayo ni baadhi ya majina ya ngeli hii: jibu-majibu, jani-majani, jeshi-majeshi, jeneza-majeneza, jambazi-majambazi, jengomajengo, jukwaa-majukwaa, jini-majini, jaribio-majaribio, jeraha-majeraha, kabati-makabati, jiwe,mawe, bega-mabega, gurudumu-magurudumu, gari-magari, dirisha-madirisha, koti-makoti, shamba-mashamba, shati-mashati, chungwa-machungwa, pera-mapera,....

**TANBIHI :** Maneno machacke katika ngeli hii uwingi wake hupatikana kwa kupachika kiambishi ma- tu, bali kwa kuondoa silabi ya kwanza na kupachika ma au me.

Mfano : Jicho = macho

Jambo = mambo Jiwe = mawe Jino = meno

**MATUMIZI YA NGELI YA LI- YA/ JI-MA**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Jahazi limezama baharini | Majahazi yamezama baharini |
| Jibu limepatikana | Majibu yamepatikana |
| Jino limeng'oka | Meno yameng'oka |
| Gari limekwama mchangani | Magari yamekwama mchangani |
| Jambazi litakamatwa jana | Majambazi yamekamatwa |

| | |
|---|---|
| Jipu litapasuliwa hospitalini | Majipu yatapasuliwa hospitalini |
| Jicho linaniuma | Macho yananiuma |
| Kabati limeingizwa chumbani | Makabati yameingizwa chumbani |

**VIVUMISHI VYA NGELI YA LI-YA-**

a)**Vivumishi vya kuonyesha**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Ganda hili linateleza | Maganda haya yanateleza |
| Ganda hilo linateleza | Maganda hayo yanateleza |
| Ganda lile linateleza | Maganda yale yanateleza |

**b)Vivumishi vya kumiliki**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Koti langu limeibwa | Makoti yetu yameibwa |
| Koti lako limeibwa | Makoti yenu yameibwa |
| Koti lake limeibwa | Makoti yao yameibwa |

**Kusisistiza**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Jipu lenyewe limeiva | Majipu yenyewe yameiva |
| Shamba lenyewe linalimwa | Mashamba yenyewe yamelimwa |

**d)Vivumishi vya kuuliza**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Jukwaa lipi tutaonyeshea? | Majukwaa yapi tutaonyeshea? |
| Jiwe lipi amekutupia? | Mawe yapi amekutupia? |
| Juma gani tutapumuzika? | Majuma gani tutapumuzika? |

**e)Vivumishi vya idadi**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Shamba moja limelimwa | Mashamba mawili yamelimwa |
| | Mashamba matatu yamelimwa |

Mashamba manne yamelimwa

Mashamba matano yamelimwa

Mashamba -sita yamelimwa

Mashamba -saba yamelimwa

Mashamba manne yamelimwa

Mashamba manne yamelimwa

**f) Vivumishi vya sifa**

| | |
|---|---|
| Jengo refu limeanguka | Majengo marefu yameanguka |
| Jiwe kubwa limepasuka | Majiwe makubwa yamepasuka |
| Kabati zuri limenunuliwa | Makabati mazuri yamenunuliwa |
| Jeneza fupi limetengenezwa | Majeneza mafupi yametengenezwa |

**NGELI YA U-**

Ngeli hii huchukua majina ya dhahania, (majina ya maarifa) kiamishi ngeli katika kitenzi ni u- katika umoja na uwingi Yafuatayo ni baadhi ya majina ambayo yamo katika ngeli hii: ulafi, uzembe, ukubwa, unene, wembamba, weusi, ujinga, ujana, ulaghai, ujuzi, uzee, utajiri, umasikini, wekundu, uchovu, ubahili, ulevi, utakatifu, uovu, ivivu, ukatili...

**MATUMIZI YA NGELI YA U-**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Ukubwa unampa kiburi | Ukubwa unawapa kiburi |
| Unene unamletea jasho | Unene unawaletea jasho |
| Weusi unampendeza | Weusi unawapendeza |
| Ujinga ulimdunisha | Ujinga uliwadunisha |
| Uzungu unampumbaza | Uzungu unawapumbaza |
| Werevu umenizidi | Werevu umewazidi |
| Utajiri unamzuaza | Utajiri unawazuaza |
| Uzembe unanichukiza | Uzembe unawachukiza |
| Utani unaniudhi | Utani unatuudhi |

**VIVUMISHI VYA NGELI YA U-**

**a) Viambishi vya kuonyesha**

Unene huu mzuri

Unene huo mbaya

Unene ule unanitia

**b) Vivumishi vya kumiliki**

Weusi wangu unapendeza

Weusi wetu unapendeza

Weusi wako unapendeza

Weusi wenu unapendeza

Weusi wake unapendeza

Weusi wao unapendeza

**c) Vivumishi vya kurejesha**

Uzuri wenyewe umemtoka

Uzuri wenyewe umewatoka

Ujuzi wenyewe ni wa kulazimisha

**d)Vivumishi vya kuuliza**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Unafiki upi unakuchukiza ? | Unafiki upi unawachukiza? |
| Ukarimu gani unazungumzia? | Ukarimu gani mnazungumzia? |
| Ujinga upi umezidi? | Ujinga upi umewazidi? |

**e) Vivumishi vya idadi** : Ngeli hii haiendani na idadi

**g) Vivumishi vya sifa**

Utajiri mkubwa

Weusi mzuri

Ujuzi mdogo

1. **NGELI YA U-I-ZI**

Majina yaliyomo katika ngeli hii hutambulishwa na viambishi ngeli **u**-na **i**- katika umoja, na **zi-** katika uwingi. Yafuatayo ni baadhi ya majina ya ngeli hii: ubao-mbao, ufunguo-funguo ukuta-kuta, wavu-nyavu, ukucha-kucha, ufagio-fagio, ufito-fito, wayo-nyayo, wimbo-nyimbo. ulimi-ndimi, uso-nyuso,.... barabara-barabara, njia-njia, alama-alama, sauti-sauti, nyumba-nyumba, suruali-suruali, akili-akili, baiskeli-baiskeli, kalamu-kalamu, karatasi-karatasi, ndege-ndege,....

**Matumizi ya ngeli hii**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Barabara imenyooka | Barabara zimenyooka |
| Baiskeli imeibwa | Baiskeli zimeibwa |
| Kalamu inaandika | Kalamu zinaandika |
| Ukuta umebomoka | Kuta zimebomoka |
| Wimbo unafurahisha | Nyimbo zinafurahisha |
| Ufunguo umepotea | Funguo zimepotea |
| Unyasi umekauka | Nyasi zimekauka |

**VIVUMISHI VYA NGELI YA U-I-ZI-**

a) **Vivumishi vya kuonyesha**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Karatasi hii imechanika | Karatasi hizi zimechanika |
| Karatasi hiyo imechanika | Karatasi hizo zimechanika |
| Karatasi ile imechanika | Karatasi zile zimechanika |
| Wavu huu umekatika | nyavu hizi zimekatika |
| Wavu huo umekatika | nyavu hizo zimekatika |
| Wavu ule umekatika | nyavu zile zimekatika |

b) **Vivumishi vya kumiliki**

| | |
|---|---|
| Ndege yangu imeanguka | Ndege zetu zimeanguka |
| Ndege yako imeanguka | Ndege zakozimeanguka |
| Ulimi wangu umeumia | Ndimi zetu zimeumia |
| Ulimi wako umeumia | Ndimi zenu zimeumia |
| Ulimi wake umeumia | Ndimi zao zimeumia |

c) **Vivumishi vya kurejesha**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Akili yenyewe imevurugika | Akili zenyewe zimevurugika |
| Suruali yenyewe imechafuka | Suruali zenyewe zimechafuka |
| Baiskeli yenyewe imeibwa | Baiskeli zenyewe zimeibwa |
| uzi wenyewe umekatika | Nyuzi zenyewe zimekatika |
| Ubao wenyewe umefutwa | Mbao zenyewe zimefutwa |
| Ufunguo wenyewe umepotea | Funguo zenyewe zimepotea |

**d) Vivumishi vya kuuliza**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Suruali ipi inakubana? | Suruali zipi zinawabana? |
| Karatasi ipi/gani imechanika? | Karatasi zipi/gani zimechanika? |
| Ndege ipi imeanguka? | Ndege zipi zimeanguka? |
| Wimbo upi umekufurahisha? | Nyimbo zipi zimekufurahisha? |
| Uso upi unakupendeza? | Nyuso zipi zinakupendeza? |
| Ukucha upi/gani umerefuka? | Kucha zipi/gani zimerefuka? |

**e) Vivumishi vya idadi**

Ndege -moja imepotea
Ndege mbili zimepotea

Ndege -tatu zimepotea

Ndege -nne zimepotea

Ndege -tano zimepotea

Ndege -sita zimepotea

Ndege -saba zimepotea

Ndege -nane zimepotea

Ndege -tisa zimepotea

Ndege -kumi zimepotea

Ndege ishirini zimepotea

a) Wembe mmoja umeibwa
Nyembe mbili zimeibwa

Nyembe -tatu zimeibwa

Nyembe- nne zimeibwa

Nyembe -tano zimeibwa

Nyembe- sita zimeibwa

Nyembe -saba zimeibwa

Nyembe -nane zimeibwa

Nyembe -tisa zimeibwa

**f)Vivumishi vya sifa**

| | |
|---|---|
| Nyumba nzuri imejengwa | Nyumba nzuri zimejengwa |
| Kalamu ndefu inaandika | Kalamu ndefu zinaandika |
| Baiskeli mpya inauzwa | Baiskeli mpya zinauzwa |
| Karata nyepesi imechanika | Karata nyepesi zimechanika |
| Ufa mkubwa umezibwa | Nyufa kubwa zimezibwa |
| Ufagio mrefu umepotea | Fagio ndefu zimepotea |
| Ubao mweusi umefutwa | Mbao nyeusi zimefutwa |

## 2. NGELI YA PA-M-KU-

Ngeli hii huchukua majina yote ya mahali. Viambishi ngeli vyake ni **pa-m-ku**- katika vitenzi. Kwa kawaida katika ngeli hii mahali panapozungumziwa panaweza kujulikana kwa ujumla (pa-), kwa wazi wazi (ku-) au pakawa ndani ya kitu (m-).

**Matumizi ya ngeli hii**

| **Umoja** | **Wingi** |
| --- | --- |
| Butare pamechafuka | Butare pamechafuka |
| Hospitalini kuna maajabu | Hospitalini kuna maajabu |
| Ziwani mna samaki | Maziwani mna samaki |
| Sokoni kuna chakula | Masokoni kuna chakula |
| Ruhengeri kuna mlima | Ruhengeri kuna milima |
| Kichwani pananiwasha | Vichwani pananiwasha |
| Mguuni pamevimba | Miguuni pamevimba |
| Kitabuni mna hadithi tano | Vitabuni mna hadithi tano |
| Msituni kuna wanyama | Misituni kuna wanyama |

**VIVUMISHI VYA NGELI YA PA-M-KU-**

***a)*** **Vivumishi vya kuonyesha**

**-pa-**

Mahali hapa pana maji

Mahali hapo pana maji

Mahali pale pana maji

**-m**-

Chumbani humu mna joto

Chumbani humo mna joto

Chumbani mle mna joto

**-ku-**

Msituni huku kuna simba

Msituni huko kuna simba

Msituni kule kuna simba

**b)Vivumishi vya kumiliki**

**-pa-**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Mahali pangu pamefagiliwa | Mahali petu pamefagiliwa |
| Mahali pako pamefagiliwa | Mahali penu pamefagiliwa |
| Mahali pake pamefagiliwa | Mahali pao pamefagiliwa |

**-m-**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Chumbani mwangu mmechafuka | Chumbani mwetu mmechafuka |
| Chumbani mwako mmechafuka | Chumbani mwenu mmechafuka |
| Chumbani mwake mmechafuka | Chumbani mwao mmechafuka |

**c)Vivumishi vya kurejesha**

**-pa-**

Mahali penyewe panaogopesha

Uwanjani penyewe panateleza

**-m-**

Ndani mwenyewe mnanuka vizuri

Mtoni mwenyewe mna mamba

**-ku-**

Nje kwenyewe kuna joto

Shambani kwenyewe kuna simba

**d)Vivumishi vya kuuliza**

Mahali papi panapendeza?

Mahali kupi kunapendeza?

Mahali mpi mnapendeza?

**e)Vivumishi vya idadi**

Mahali pamoja

Mahali pawili

Mahali patatu

Mahali panne

Mahali patano

Mahali sita

Mahali saba

Mahali kumi

Mahali vya pengi

**f)Vivumishi sifa**

Mahali pachafu patafagiliwa

Mahali kuchafu kutafagiliwa

Mahali mchafu mtafagiliwa

Sokoni pasafi patauzwa chakula

3. **NGELI YA KU-**

Ngeli hii inaainisha vitenzijina, yaani majina yanayo umbo la kitenzi kama, kuimba, kucheza, kucheka , kulima, kujifunza,...

**Matumizi ya ngeli hii.**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Kucheza kumemchokesha | Kucheza kumewachokesha |
| Kuimba kunamfurahisha | Kukimbia kunawafurahisha |
| Kusali kutamfariji | Kusali kutawafaraji |
| Kulewa kumemponza | Kulewa kumewaponza |

**Vivumishi vya kuonyesha**

Kuimba huku kubaya.

Kulima huko kutawachokesha

Kunywa kule kunalevya

**Vivumishi vya kumiliki**

Kukimbia kwangu kumepungua.

Kuimba kwako kumetufurahisha.

Kunywa kwake kumemuua.

Kukimbia kwetu kumepungua.

Kuimba kwenu kumetufurahisha.

Kunywa kwao kumewaua.

***a)*** **Vivumishi vya kurejesha**

Kusali kwenyewe kumekwisha.

Kusoma kwenyewe kubaya.

kunywa kwenyewe kumezidi.

***b)*** **Vivumishi vya kuuliza**

Kuvaa kupi kunapendeza?

Kuandikwa kupi kunatakiwa?

Kuimba gani kutashinda?

***c)*** **Vivumishi vya sifa**

Kuimba kuzuri kumesifiwa.

Kucheza kubaya kumekwisha.

Kutembea kurefu kumetuchokesha.

**Marejeleo:**

1. Ahmed Ndalu , Mwangaza wa Kiswahili( 1997), Nairobi, East African Educational Publishers
2. D.P.B. Massanba, Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu Sekondari na Vyuo(2001)Dares-salaam, TUKI.
3. Sylvain Ntawiyanga na Jacqueline, Kiswahili kwa Shule za Rwanda, Kitabu cha mwanafunzi, Kidato cha Pili( 2016),Kigali, Longhorn Publishers
4. TATAKI , Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la Tatu (2014), Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, Oxford University Press.
5. Intaneti